



## **TAMKO LA KULAANI KUUMIZWA NA KUDHALILISHWA KWA VIONGOZI WA WANAWAKE WA CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO (CHADEMA)**

Mtandao wa Kupambana na Ukatili wa Kijinsia nchini Tanzania (MKUKI) pamoja na Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu (CWHRDs); na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kupigwa viongozi wabunge wanawake wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA); Mheshimiwa Halima Mdee (MB), Mheshimiwa Esther Bulaya (MB) pamoja na wanachama na wafuasi wengine.

Taarifa tulizozipata kupitia vyombo vya habari pamoja na kuwasiliana na waathirika moja kwa moja ni kwamba mnamo tarehe 13 mwezi Machi saa saba mchana viongozi hao walienda gereza la Segerea kumpokea kiongozi wao, mheshimiwa Freeman Mbowe (MB). Taratibu zote za kisheria ikiwa na pamoja na hati ya kumtoa mheshimiwa Freeman Mbowe zikiwa zimefuatwa.

Hata hivyo walipofika, geti la kwanza kuingia gerezani walizuiliwa na ndipo walianza kugeuza magari yao kurudi uraiani.

Wakiwa wanatoka, askari wa gereza alipiga filimbi kuonesha hali ya hatari, kitendo ambacho kilipelekea maaskari wa gereza kuja kwa wingi na kuanza kuwapiga na kuwadhalilisha. Mbaya zaidi, vitendo hivi vilifanywa na askari magereza wengi wao wakiwa askari wanaume.

MKUKI, CWHRDs na THRDC tunalaani vikali kitendo cha kuwapiga raia na hasa hawa viongozi wanawake kwani ni vitendo vya kiuhalifu dhidi ya binadamu, jinai kwa mujibu wa sheria za nchi na ni uvunjifu wa haki za binadamu, hususani haki za wanawake.

Ikumbukwe kuwa nchi yetu ni huru na inafuata misingi ya haki za binadamu. Pia nchi yetu ni mwanachama wa Mikataba mbalimbali ya haki za binadamu kimataifa na kikanda. Tanzania imeridhia Mikataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966. Mikataba wa Banjul wa Afrika juu ya haki za Binadamu na Mikataba wa Roma unaoanzisha Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC) na mengine mingi. Mikataba hii inaitaka nchi

wanachama kufanya jitihada za makusudi kwa mujibu wa sheria na taratibu za kiuongozi kuhakikisha zinatoa haki kwa raia, hususani haki ya ulinzi wa utu wa mtu, haki ya kufuata utaratibu wa kisheria (due process), haki ya uhuru dhidi ya utoaji adhabu ya mateso na kutweza utu wa binadamu na haki ya kutotumia nguvu dhidi ya raia. Zaidi, kwa mujibu wa Mkataba wa Roma, uvunjifu wa haki hizi, hususani haki ya kutumia nguvu dhidi ya raia ni sehemu ya uhalifu dhidi ya ubinadamu (crime against humanity).

Pamoja na Mikataba hii, pia kuna mikataba mahususi inalinda haki za wanawake. Mithalani Mkataba wa Jinsia na Maendeleo Afrika wa Nchi za Kusini Mwa Afrika, Maputo Protoko na Mkataba wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW). Nchi yetu pia imekuwa kinara wa kusimamia maazimio ya Tamko la Beijing.

MKUKI, CWHRDs na THRDC, tumefadhaishwa sana na ukatili waliofanyiwa viongozi wanawake hasa ukizingatia tupo katika kipindi cha kutathmini utekelezaji wa maazimio ya Beijing wa miaka 25 pamoja na kwamba huu ni mwezi wa kusherehekea michango ya wanawake katika kuleta na kudumisha amani na maendeleo nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 14 na 15 inaeleza kuwa "Kila mtu anayo uhuru wa kukusanyika kwa uhuru na amani. Katiba inaelekeza zaidi kuwa "Kila mtu ana haki ya kuishi na ulinzi wa maisha yake kwa mujibu wa sheria." Zaidi ya haki, Katiba inaelekeza kuwa "Kila mtu anastahili kuheshimu na kulindwa utu wake", na kwamba serikali " kuweka taratibu za kisheria kuhusu hali, njia na kiwango ambacho haki ya usalama wa mtu inaweza kuingiliwa bila kuathiri masharti ya katiba.

Vyombo vya dola vina wajibu wa kulinda raia na pia kuchukua hatua stahiki pale kunapokuwa na uvunjifu wa amani. Tunatambua maelekezo ya Sheria ya Magereza Sura 58, Mwenendo wa makosa ya Jinai Sura 20 na Sheria ya Polisi na Nguvu ya Ziada, Sura 322, juu ya matumizi ya nguvu kuzuia kutoroka kwa wafungwa au walioko chini ya ulinzi na kukwepa kukamatwa. Sheria hizi zimeelekeza hatua za kufuatwa, mathalani onyo kutolewa, na kama kuna ulazima huo na lengo kuwa kumuweka mtuhumiwa chini ya ulinzi, sio kutesa au kutweza utu wake baada ya kumkamata.

Hivi karibuni tumeshuhudia nguvu kubwa inayotumika kufifisha haki ya uhuru wa wananchi kukusanyika na kutoa mawazo yao. Tumeshuhudia pia jinsi wanawake viongozi wa siasa kutoka vyama vya upinzani wanavyodhalilishwa na pia nguvu kubwa sana inayotumika ambayo ni kinyume na utawala wa sheria